JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 19- 2019/2020**

**DHIDI YA**

# MWANANCHI NEWSPAPER

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 **Kwamba**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **Mwananchi Newspaper** tarehe 25 Mei, 2018, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

1.2 **Kwamba,** kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yeyote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 **Kwamba**, tarehe 13/04/2020, **Mwananchi Newspaper** kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii inatuhumiwa kuchapisha na kutangaza taarifa yenye kupotosha na kuleta mkanganyiko kwa jamii.

1.4 **Kwamba, Mwananchi Newspaper** ilitangaza habari hizo bila kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi wa Habari, kwa sababu mhariri wa kurasa hizo aliweka/alichapisha picha jongefu yenye kichwa cha habari, **"RAIS MAGUFULI AKINUNUA SAMAKI SOKONI MJINI CHATO"** huku wakiweka picha jongefu iliyochukuliwa mnamo 3 Juni 2019 ambapo **Mhe. Rais Dr. John Joseph Pombe Magufuli** alikuwa akinunua samaki katika soko la Feri, Dar es Salaam jambo ambalo ni la kupotosha jamii na kuleta hisia hasi hususani katika kipindi hiki ambapo Taifa na Serikali kwa ujumla iko katika harakati za kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-19).

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

**Kwamba,** kitendo cha kuchapisha na kutangaza habari hizo ambazo hazina ukweli na za kupotosha jamii, **Mwananchi Newspaper** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 5 (1) (a), na 12 (l) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

*5.-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*

*(a) Ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

*12.-Online content services provider shall not publish-*

*(l) false content which is likely to mislead or deceive the public unless where it is clearly pre- stated that the content is –*

*(i) satire and parody*
*(ii) fiction; and*
*(iii) where it is preceded by a statement that the content is not factual*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 15 Aprili, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Mwananchi Newspaper**, wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 15 Aprili, 2020 saa 09:00 alasiri, uongozi wa **Mwananchi Newspaper** ukiongozwa na Bw. Boniface Meena, Msimamizi wa Maudhui Mtandaoni wa **Mwananchi Newspaper** ambaye aliambatana na Bw. Joseph Kesagero, Mkurugenzi wa Sheria wa **Mwananchi Newspaper**, walifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao.

## 4.0 Kuangalia Maudhui ya Mwananchi Newspaper

Kamati ya Maudhui pamoja na Uongozi wa **Mwananchi Newspaper** walipata fursa ya kuangalia maudhui yaliyochapishwa katika kurasa za mitandao ya kijamii ya gazeti hilo tarehe 13 Aprili, 2020 ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au la.

## 5.0 Maelezo ya Utetezi ya Mwananchi Newspaper

Uongozi wa **Mwananchi Newspaper**, ukiongozwa na Bw Boniface Meena, ulitoa utetezi wao na kusema kuwa tarehe 13/04/2020 mmoja wa waandishi wao mwandamizi (senior reporter) alituma katika Kundi lao la "*WhatsApp*" picha jongefu iliyokuwa inamuonyesha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akiwa sokoni akinunua samaki na kudai kuwa alikua sokoni huko wilayani Chato.

Baada ya kupata habari/picha jongefu hiyo waliichapisha katika kurasa za mitandao ya kijamii ya "*tweeter*" na "*instagram*" *ya* ***Mwananchi Newspaper*** wakieleza kuwa Rais Magufuli yuko sokoni mjini Chato akinunua samaki, kwa sababu waliamini kuwa ni taarifa ya kweli na sahihi. Bw. Meena alisema waliamini taarifa hiyo ni ya kweli kwa sababu aliyeileta kwenye kundi lao la *WhatsApp* ni mwandishi wao mwandamizi na pia ni mwenyeji wa Mjini Chato.

Bw. Meena aliendelea kuiambia Kamati kuwa baada ya muda kidogo mwandishi huyo alitoa maelezo katika kundi la *WhatsApp* na kusema kuwa taarifa hiyo haikuwa sahihi.

Baada ya maelezo hayo, waliamua kuifuta habari hiyo, na kisha walimhoji kwa nini alituma taarifa isiyo sahihi. Mwandishi huyo aliwajibu kuwa aliipata habari/picha jongefu hiyo kutoka katika Kundi lingine. Na walipozidi kumhoji kwa nini hakuhakiki ukweli wa taarifa hiyo alikosa majibu.

Halikadhalika, Bw. Meena aliendelea kuieleza Kamati kuwa baada ya kuona mtoa taarifa alikosa majibu ya kuridhisha, iliwabidi kuomba radhi kwa Rais na wote walioathirika na taarifa hiyo, kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za **Mwananchi Newspaper** na kuahidi kuchukua hatua kali dhidi ya waliohusika kufanya upotoshaji huo.

Aidha, Bw Meena aliiambia Kamati kuwa wamekwisha chukua hatua za kinidhamu kwa wahusika wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na kusitisha mkataba wa ajira wa mtoa habari huyo, pia mtengenezaji wa Maudhui aliye chapisha picha jongefu hiyo amepewa onyo kwa kutenda kosa hilo. Halikadhalika Bw. Meena mwenyewe amepewa onyo na karipio.

Bw. Meena aliendelea kusema kuwa kosa hilo ni la kibinadamu na waliiomba radhi Kamati.

Bw. Meena aliendelea kusema kuwa wamechukua hatua kutokana na jambo hilo, ambapo tarehe 14/04/2020 waliitisha kikao cha nidhamu ambapo mtoa taarifa alihojiwa na hatimaye yalitolewa maamuzi ya kusitisha mkataba wa ajira yake.

Kwa upande wake, Bw. Josephat Joseph Kasegero (ambaye ni Meneja wa Sheria wa Mwanachi Newspaper) alisema kuwa wao kama kampuni hawana ubishi juu ya kilichotokea kwa sababu kwa chombo cha habari kufanya jambo kama hilo lililotokea ni mwenendo mbaya sana (serious missconduct) na hivyo wao wanaiomba radhi Kamati kwa kilichotokea na kwamba watachukua tahadhari ili jambo kama hilo lisitokee tena.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Baada ya kusikiliza utetezi wa **Mwananchi Newspaper** Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Mwananchi Newspaper** imechapisha maudhui yenye lengo la kupotosha jamii hasa kwa kutokuzingatia Sheria, Weledi na Misingi ya Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

6.2 Kamati imeona kuwa hoja ya kuwa walichapisha habari hiyo wakijua ni sahihi kwa vile ilitumwa kwenye kundi la *WhatsApp* wanaloliamini na ilitumwa na mtu ambaye ni mwandishi wa habari mwandamizi na pia mwenyeji wa Chato haina nguvu na inaonesha kuwa kuna ombwe katika usimamizi na uhariri wa habari.

Pia Mhariri alipaswa ajiulize kama kweli Mjini Chato kuna Soko la samaki au la. Ukosefu wa usimamizi mahiri wa maudhui ndani ya **Mwanachi Newspaper** ndio unaufanya uongozi wake kusema mbele ya Kamati kuwa hata na wao wanashangaa ni kwa nini mtu huyo alituma habari hiyo ya kupotosha kwenye kundi hilo la *WhatsApp*, huku wakishindwa kujiuliza kwa nini na wao waliiamini taarifa hiyo bila kujiridhisha kuhusu ukweli na uhalisia wa tukio hilo.

6.3 Kamati ya Maudhui imejiridhisha kuwa **Mwananchi Newspaper** kama chombo cha habari cha kuaminika na chenye hadhi, kimefanya kosa la kuchapisha kwa uzembe maudhui yenye kupotosha jamii na yenye kuleta hisia hasi juu ya nia njema ya Mhe. Rais na Serikali kwa ujumla katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19).

**Mwananchi Newspaper** ilitakiwa kuwa makini na kuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi wa Habari kwa kuangalia madhara ya habari waliyochapisha ambayo kwa taswira yake inadhoofisha jitihada za Serikali katika kupambana na janga hili la ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-19).

6.4 Kamati imebaini kuwa **Mwananchi Newspaper** ina ombwe la usimamizi na uhariri wa maudhui wanayopakia mtandaoni jambo linalopelekea kuchapisha kila habari wanayotumiwa na waandishi wao kwa kigezo tu cha kuwa habari hiyo imeletwa katika kundi lao la *WhatsApp* wanaloliamini bila ya kujiridhisha kuhusu ukweli na uhalisia wa habari husika.

6.5 Kamati imepokea taarifa ya hatua iliyochukuliwa na **Mwananchi Newspaper** baada ya kosa kutendeka kwa kuondoa habari hiyo ili isiendelee kusambaa na kuzidi kupotosha umma. Halikadhalika hatua ya kuomba radhi baada ya kugundua makosa yao pia imezingatiwa. Hata hivyo Kamati imeona kuna madhara makubwa yaliyosababishwa na habari hiyo kijamii.

## 7.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Mwananchi Newspaper**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Mwananchi Newspaper** kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

**Hivyo Basi**, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya mwaka

2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo dhidi ya **Mwananchi Newspaper:-**

1. Kusitishwa utoaji wa huduma ya maudhui mtandaoni kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia leo kwa ukiukaji wa Kanuni kama ilivyoainishwa katika shauri hili, ili waweze kujirekebisha. Kamati imefikia uamuzi huu kwa lengo la kuwapa fursa **Mwananchi Newspaper** kujitambua, kujitafakari na kujipanga vizuri zaidi ili waweze kuendesha kituo chao kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taaluma ya habari na utangazaji; na

2. Kulipa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **16 Aprili 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

Uamuzi huu umesainiwa na:

**Bw. Joseph Method Mapunda**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI WAFUATAO:**

**Bw. Abdul Ramadhani Ngarawa.........................................**

**Bw. Jacob Gregory Tesha................................................**